



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb. Na. NDC/I.20/6/VOL.VII/190

14/05/2024

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA WA MUDA YA UKAGUZI WA MAPATO KWENYE MAGETI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia nafasi 19 za kazi za Mkataba wa Muda ya Ukaguzi wa Mapato Magetini na anakaribisha maombi kwa watanzania wote wenye sifa na uwezo kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi kama ilivyo orodheshwa katika tangazo hili. Aidha mnajulishwa kuwa mwisho wa maombi haya ni tarehe 27/05/2024.

### 1. MKAGUZI WA MAGETINI - NAFASI 19

#### (a) Sifa za mwombaji.

Mwenye elimu ya kidato cha nne au sita, aliyefaulu somo la Hisabati.

#### Kazi na majukumu

- Kuhesabu na kuhakiki ili kujiridhisha kuwa mzigo uliopakiwa kwenye chombo cha usafirishaji umelipiwa ushuru wa Halmashauri na unastakabadhi halali ya Serikali inayolingana na tozo stahiki.
- Kutunza Kumbukumbu za magari yote yaliyobeba mazao ya misitu, mazao ya biashara na chakula yanayopita kwenye kizuizi (geti) cha Halmashauri.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kijiji ambapo geti lipo na kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Barabara ya Lupembe – Kidegembye (Kata ya Kidegembye Kijiji cha Kidegembye), SLP 547 Njombe, Simu: +255 26 2782111 (Mkurugenzi), +255 26 2782027 (Maulizo), Nukushi +255 26 2782857 Barua pepe: info@njombedc.go.tz; Tovuti: www.njombedc.go.tz


## 2. MAELEKEZO

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wasiozidi umri zaidi ya miaka 45 na wasiopungua umri wa miaka 18.
- ii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI,
- iii. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
  - a) Cheti cha mihani wa kidato cha nne au sita.
  - b) Cheti cha kuzaliwa.
  - c) Picha mbili za passport size za hivi karibuni.
- iv. Hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (Result slip) na "Transcript" hazitafanyiwa kazi.
- v. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au kingereza.
- vi. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
- vii. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe **27/05/2024** saa **9:30** alasiri, baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri [www.njombedc.go.tz](http://www.njombedc.go.tz) na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri.

Barua zote zitumwe kwa:-

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE,  
S.L.P 547,  
**NJOMBE.**

Tangazo hili limetolewa na:-

  
Christopher A. Sanga  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
**NJOMBE**

Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya  
NJOMBE